

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

15 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 15 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

230. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa muda mrefu sasa Wilaya ya Kilindi haina Hospitali ya Wilaya lakini wanayo Hospitali ya Rufaa inayomilikiwa na

Kanisa la KKKT lakini Watumishi wote na huduma zote za Hospitali hiyo zinagharamiwa na Halmashauri ya Wilaya (DED) na wao (KKKT) wanamiliki majengo:-

Je, Serikali haioni imefika wakati wa kufanya makubaliano ya kununua Hospitali hiyo ili kupunguza gharama kwa Serikali ya kujenga Hospitali ya Wilaya.

231. MHESHIMIWA DKT. JASMINE TISEKWA BUNGA (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara zinazotoka Kidiwa hadi Tandali, Daraja la Mgeta hadi Lukuyu, Visomolo hadi Lusungi na Langali SACCOS hadi Shule ya Sekondari Langali Tarafa ya Mgeta Wilayani Mvomero zimejengwa kwa nguvu za Wananchi lakini bado hazipitiki kutokana na vikwazo vya miundombinu na madaraja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hizo ili kuondoa adha wanazopata Wananchi.

WIZARA YA NISHATI:

232. MHESHIMIWA ALLAN JOSEPH KIULA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza mpango kabambe wa kusambaza umeme Vijiji chini ya mpango wa REA:-

- 
- (a) Je, ni lini Vijiji vyote 70 vya Wilaya ya Mkalama vitapata umeme wa REA II;
 - (b) Je, Serikali ipo tayari kuweka umeme katika Vitongoji vinavyopitiwa na njia ya umeme wa REA.

233. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Wananchi wanaoishi katika Jimbo la Kibiti hutumia nishati ya mkaa na kuni kwa matumizi ya Nyumbani, Shuleni, Gerezani n.k hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kukata miti ovyo:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka nishati mbadala;

(b) Je, ni aina gani ya nishati itakayotumika badala ya kuni na mkaa.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

234. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara ya Ziba – Puge na Ziba – Choma kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za usanifu wa barabara hizo na hatimaye kuanza ujenzi ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

235. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya Wananchi

ambao maeneo yao yametwaliwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ) pasipo kulipwa fidia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kulipa fidia kwa Wananchi hao.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**236. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana kwenye suala la ubakaji (SOSPA) ya mwaka 1998 na marekebisho yaliyofanywa mwaka 2017 yote yana lengo la kukomesha vitendo vya ubakaji wa Watoto chini ya miaka 18 na Wanafunzi (kifungo miaka 30) na Watoto chini ya miaka 10 (kifungo cha maisha):-

- (a) Je, tokea kupitishwa kwa Sheria hii (SOSPA) na marekebisho yake, ubakaji umepungua au kukoma hapa nchini;
- (b) Je, kama bado changamoto ipo, Serikali ina mpango mkakati gani mpya katika kupambana kutokomeza ubakaji Tanzania.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

237. MHESHIMIWA LUCY SIMON MAGERELI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Sera ya *cost sharing* ilianzishwa ili kuisaidia Serikali kibajeti katika maeneo ya Afya na Elimu, hadi leo ni bayana kuwa Sera hii imeshindwa na hatimaye Serikali kurejea tena katika kugharamia Elimu ya Msingi na Sekondari:-

- - (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Elimu ya Tanzania ambayo imeporomoka sana katika Shule za Umma inakuwa yenyewe ubora unaotarajiwa;
 - (b) Je, Serikali inafanya nini kuhusu madai ya stahiki za Walimu ambazo hazijalipwa kwa muda mrefu sasa.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

238. MHESHIMIWA HASSAN ELIAS MASALA (NACHINGWEA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, nini mpango wa Serikali juu ya kuboresha jengo la Mahakama Wilayani Nachingwea.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)



DODOMA
15 MEI, 2019

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE